# Uwekezaji wa mabilioni kufungua sekta ya uvuvi



WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa akiwa katika Uzinduzi wa Mpango kabambe wa Sekta ya Uvuvi wa miaka 15.



Wavuvi wa soko la Kimataifa la Samaki Feri, wakipakuwa samaki kutoka katika boti za uvuvi.



Mchuuzi akiwa amabeba samaki katika Soko la Kimataifa la feri.

Na ASHURA ASSAD

SIFA kubwa ya kiongozi ni ufuatiliaji wa maendeleo kwa wananchi ndiyo maana viongozi wengi wazuri, pamoja ya kuwa na wasaidizi katika kazi zao, lakini huwa na tabia ya kufanya ziara mara kwa mara ili kushuhudia kile kinachoelekezwa na serikali kama kinafanyika.

Hivi karibuni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alizindua Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi, ambao utakuwa kuwa dira ya maendeleo ya uvuvi kwa kipindi cha miaka 15.

Katika uzinduzi huo, waziri mkuu alitoa maagizo mbalimbali yenye lengo la kuimarisha maendeleo ya kukuza uchumi wa sekta ya uvuvi kwa lengo la kuongeza pato la taifa kupitia wizara ya mifugo na uvuvi.

Uvuvi ni miongoni mwa sekta zenye mchango mkubwa, katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini nchini.

Sekta hii inatoa ajira kwa Watanzania milioni 4.5 katika mnyororo wa thamani, ambapo ajira za moja kwa moja kwa wavuvi ni 194,804 na wakukuza viumbe maji ni 31,998.

Sekta hii huchangia kuongeza usalama wa chakula na lishe kwa asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama pia ni chanzo cha fedha za kigeni.

Shughuli za uvuvi zinafanywa zaidi na wavuvi wadogo katika maji ya asili, ambapo huchangia asilimia 95 ya samaki wote waliovuliwa nchini.

Akizungumza katika uzinduzi huo Waziri Mkuu Majaliwa, anasema sekta ya uvuvi inachangia pato la taifa kiasi cha asilimia 1.8 kwa mwaka.

Waziri Mkuu Majaliwa anasema mpango kabambe wa sekta ya uvuvi wa miaka 15, kuanzia 2021/2022-2036/2037, utakaogharimu kiasi cha dola za kimarekani milioni 132.665 (wastani sh bilioni 305.129), ambapo matarajio mpango huo uwe ni mkombozi wa sekta hiyo.

> **Mwaka 2021 wavuvi wapatao 194,804 walitumia vyombo takribani 57,991 na kuvua kiasi cha tani 477,019 zenye thamani ya sh.trilioni 2.78. Katika kipindi hicho tani 42,302 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 181,268 wenye thamani ya sh.bilioni 414 waliuzwa nje ya nchi na kuingizia serikali mrabaha wa sh.bilioni 18.4 ,"**
>
> Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki

Pia anawataka wale wote, ambao wanahusika na sekta hiyo kusimamia kwa ukaribu mpango huo, ili uweze kuleta mtazamo chanya katika sekta hii na kuongeza pato la taifa.

Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, inatekeleza ilani yake kwa vitendo lengo ni kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya uvuvi, ili kuwa na uhakika wa usalama wa chakula na lishe.

"Kupitia utajiri mkubwa wa rasilimali maji tuliobarikiwa na Mungu rasilimali hizi zinatakiwa kulindwa, kutunzwa, kusimamiwa, kuendelezwa na kuhifadhiwa na kutumi kwa njia endelevu ili ziweze kuchangia kikamilifu katika kutoa ajira, kipato,chakula na lishe ili ziweze kuchangia pato la taifa,"anasema.

Anasema uchumi wa buluu ambao unahusisha bahari ni mkombozi wa wananchi, kama ikitumika vizuri bahari na mazingira yake kuwa chanzo kikubwa cha mapato nchini.

"Badala ya mvuvi kupata kilo mbili kwa sababu hawezi kufika katika kina kirefu, kwa sasa wanatakiwa wawezeshe kufika katika kina hicho na wawe na nyavu stahiki za kuvua samaki na ule uvuvi wa nyavu zisizo stahiki unaoharibu mazingira uashwe mara moja,"anasema.

Mpango huo unatarajiwa kuleta muelekeo mzuri kwa wavuvi na kusimamiwa na wizara kuhakikisha wanawafuatilia wale walio katika sekta hii na wale ambao hawajaingia wahakikishe wanaingia na kujipanga, ili wanufaike na rasilimali hii.

**MATARAJIO YA MPANGO**

Anasema mpango huo unajumuisha katika mali asili na kuwawezesha wavuvi wadogo na kuzingatia teknolojia ya kisasa katika shughuli zao, kuongeza uzalishaji, kufanya maboresho na utafiti na kutoa elimu ya ugani ya ukuzaji viumbe bahari.

Anaeleza lengo ni kuimarisha miundombinu ya uvuvi na upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani, ili kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi.

Anasema Rais Samia amejenga mazingira mazuri ya uwekezaji, hivyo tunatakiwa kuitumia fursa hiyo, kuwaalika na waungane na Watanzania walio katika sekta ya uvuvi, ili kuondoa tatizo hilo.

"Tunaona ulaji wetu wa samaki sio mkubwa tunakula kilo 8.5 kwa mwaka kwa mtu mmoja usahihi, kila mmoja anatakiwa kula kilo 20.5 kwa mwaka sasa sijui kama mbogamboga ziko nyingi au samaki hawatoshi au bei iko juu,"anaeleza.

**MANUFAA YA MPANGO KWA MIAKA 15**

Anasema' itasaidia kukuza sekta ya uvuvi na kukuza pato lake katika mchango wa pato la taifa kufikia asilimia 10 kwa mwaka, kutoka mchango wa sasa wa asilimia 1.8 ni maendeleo yanatakiwa kwenda kwa kasi chini ya wizara.

Kuongeza mazao ya uvuvi kutoka tani 473,592 hadi kufikia 676 sawa na ongezeko la asilimia 35, ndiyo mkakati uliowekwa kwa kusimamia utekelezaji.

"Tunatakiwa kujipanga kuongeza ulaji wa samaki ili kila mtu afikie kula kilo 20.5 kwa mwaka tunatakiwa kujitathmini kila mtu akila samaki awe anaandika, ili mwaka ukiisha ajue amekula kilo ngapi,"alisema.

Vilevile kuongezeka kiwango cha samaki na mazao ya uvuvi yaliyochakatwa kusafirishwa nje ya nchi kwa asilimia 30.

Anasema mikoa yote yenye fursa za maji, wapatiwe elimu na mafunzo ya uvuvi na mazao ya uvuvi, wananchi wajifunze ili wafanye shughuli zao kwa tija na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi.

Anawataka maofisa ugani kujipanga vizuri kuwasaidia wavuvi, ili wafanye kazi wakiwa na uhakika wa kufanya kitaalamu, mpango huo utakuwa chachu ya kuendeleza sekta ya uvuvi.

**MAZINGATIO KWA WIZARA**

Wizara,taasisi,mamlaka za serikali za mitaa, taasisi binafsi na mashirika ya dini na wadau wa maendeleo, wanatakiwa kuupokea mpango huo.

Wakuu wa mikoa, wilaya wakurugenzi na watendaji wote nchini kuendelea kutoa elimu ya uvuvi, ili kuendesha shughuli za uvuvi kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo, ili kuhakikisha shughuli za uvuvi zinakuwa bora .

Hali hii inawafanya wavuvi wengi kuacha shughuli zao kwa sababu ya tozo kuwa kubwa na kukosa faida, eneo la uvuvi liendelee kuimarishwa kwa manufaa ya taifa.

Wizara inatakiwa kuandaa mawasiliano na mkakati kwa lugha nyepesi ili kila mwananchi aweze kufahamu na kuelewa kila mtu.

Wizara kuanzisha kampeni ya ufugaji samaki kwa wananchi ili kila mtu aweze kufuga samaki kwa biashara na chakula sambamba na teknolojia mpya kutambulishwa kwa wananchi ili waweze kuifahamu.

"Wizara endeleeni kuweka msukumo na kusimamia taratibu za ujenzi wa ile bandari ya uvuvi, inayojengwa kule Kilwa wilayani Lindi, mradi huo ni wa kimkakati ambao unajenga bandari ya kwanza,"anasema.

Pia anaitaka wizara hiyo kushirikiana na wadau mbalimbali kuangalia namna ya kuandaa mashamba makubwa ya uvuvi, yasiyotumia gharama kubwa ili kuzalisha samaki kwa tija.

"Hivi karibuni nilienda nchini Misri nikapelekwa sehemu kuangalia teknolojia ya uzalishaji wa samaki, wenzetu wana mashamba makubwa, ambayo wameyachimba bila kuyajenga, lakini sisi tumekuwa tukitumia gharama kubwa kuyajengea kwa mawe na kuyaweka maji, sasa inabidi tuangalie namna ya kujenga mashamba yasiyokuwa na gharama, "anaeleza.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, anasema shughuli ya uvuvi inafanywa zaidi na wavuvi wadogo kwenye maji ya asili, ambapo huchangia takribani asilimia 95 ya samaki wote wanaovuliwa nchini.

"Mwaka 2021 wavuvi wapatao 194,804 walitumia vyombo takribani 57,991 na kuvua kiasi cha tani 477,019 zenye thamani ya sh.trilioni 2.78. Katika kipindi hicho tani 42,302 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 181,268 wenye thamani ya sh.bilioni 414 waliuzwa nje ya nchi na kuingizia serikali mrabaha wa sh.bilioni 18.4 ,"anasema.

Ndaki anasema mpango huo utasaidia kuboresha sekta hiyo, ili kuwa na uvuvi endelevu wenye ufanisi kwa muktadha wa kupunguza umaskini na ukosefu wa ajira na kuongeza uzalishaji, usalama wa chakula na pato la taifa.

Anasema ili mpango huo utekelezwe kwa mafanikio na matokeo yanayoonekana, kiasi cha sh. bilioni 311.75 kwa mwaka kinahitajika, ambapo uvuvi katika maji ya asili inahitajika sh. bilioni 151.3 na ukuzaji wa viumbe maji sh.bilioni 160.45.

Anasema mpango unalengo la kuzalisha tani 600,000 za mazao ya samaki kwa mwaka, nchi nzima na hadi kufikia mwaka 2037 sekta ya uvuvi imejipanga kuchangia pato la taifa kwa asilimia 10 kutoka asilimia 1.8 iliyopo sasa.

> **Tunatakiwa kujipanga kuongeza ulaji wa samaki ili kila mtu afikie kula kilo 20.5 kwa mwaka tunatakiwa kujitathmini kila mtu akila samaki awe anaandika, ili mwaka ukiisha ajue amekula kilo ngapi**
>
> Rais Samia Suluhu Hassan.

**UMUHIMU WA SEKTA YA UVUVI**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia sekta ya Uvuvi Dk.Rashid Tamatamah, anasema umuhimu wa sekta ya uvuvi unajidhihirisha katika kuchangia uchumi wa Taifa, lishe bora na ajira kuanzia katika ngazi ya familia.

Anasema zaidi ya watu milioni nne wameendelea kunufaika na sekta ya uvuvi ikiwamo uchakataji wa samaki, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi, biashara ndogondogo na mama lishe.

Anasema changamoto zinazowakabili wawekezaji katika sekta ya uvuvi ni pamoja na upungufu wa maofisa ugani wa uvuvi ukilinganisha na mahitaji, upatikanaji wa vifaranga bora vya samaki.

Anasema serikali itaendelea kupambana na changamoto ya uvuvi haramu, ili kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinaboreka na hivyo kuchangia katika uchumi wa nchi.

**MCHANGO KATIKA VIWANDA**

Pamoja na changamoto katika sekta hii, ni ukweli usiopingika kwamba unapozungumzia Tanzania ya viwanda, huwezi kuacha kuitaja sekta ya uvuvi kama moja ya mzalishaji mkubwa wa malighafi za viwanda hususan vile vya nyama na usindikaji kwa jumla.

Katika mwaka 2016/2017, tani 39,691.5 za samaki na mazao ya uvuvi yenye thamani ya sh,526.99 bilioni yaliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa sh. bilioni 14.30 kama ushuru.

Anasema serikali imeimarisha udhibiti ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ili kulinda soko la ndani na nje ya nchi, kwa kutumia maabara ya taifa ya uvuvi ya Nyegezi mkoani Mwanza.

**MKAKATI DHIDI YA UVUVI HARAMU**

Anasema serikali imezindua mkakati unaolenga kutokomeza uvuvi haramu, kwa kuanzisha operesheni ya kutumia ndege maalumu itakayofanya doria katika eneo la bahari kuu, ili kudhibiti eneo hilo.

"Changamoto ya uvuvi haramu ni kubwa, mtu anapiga bomu katika matumbawe anafanya uharibifu, ambao kuyatengeneza tena yanachukua zaidi ya miaka 100, huku yeye akiharibu kwa dakika tano, " anaeleza.

Anasema kutokana na teknolojia hii ya kisasa ya kutumia ndege katika doria, itasaidia kudhibiti kabisa uvuvi haramu katika ukanda wa nchi za Kusini Magharibi.

Anabainisha kuwa lengo la kuchukua hatua hiyo, ni kuwezesha samaki wengi kuzaliana, ili lengo la serikali la kujenga viwanda vya kusindika mazao ikiwemo viwanda vya kusindika minofu ya samaki lifanikiwe.

**WADAU WA UVUVI WAONGEA**

Hussein Juma Mkazi wa Kigamboni anasema uzinduzi kabambe wa sekta ya uvuvi wa miaka 15, ukalete mafanikio makubwa ili kuhakikisha rasilimali za baharini zinalindwa na kuweka aina ya uvuvi utakaozingatia mazingira bora na kulinda mazao ya bahari ikiwemo matumbawe.

Anasema matumbawe ya baharini ambayo ni mazalia ya samaki, yapo katika tishio la kutoweka kutokana na uharibifu unaosababishwa na wavuvi haramu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Uvuvi Tanzania, Profesa Yunus Mgaya, anasema mpango huo utaleta maendeleo katika sekta ya uvuvi kwa kipindi cha miaka 15.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Tipo Nyabenyi, anasema wamefurahi kushirikishwa na serikali katika mpango huo muhimu, ambao utaleta tija katika sekta ya uvuvi na kutokomeza uvuvi haramu.

Anasema sekta ya uvuvi ikiimarishwa na kusimamiwa inaweza kuleta mabadiliko makubwa, kwa kuongeza mchango katika pato la taifa na kukuza biashara ya samaki nchi za nje.

He said Tanzania is a country to be

The economy will grow further to 6.6

TURN TO PAGE 2

The Guardian

# Livestock registration nears end, cattle keepers facing fines, losses

By Guardian Reporter, Dodoma

LIVESTOCK branding and registration using electronic earrings is set to be closed at the end of the month, the Livestock and Fisheries ministry has said.

Prof Hezron Nonga (pictured), the director of livestock services, told a press conference yesterday that thereafter animal keepers who failed to meet the deadline will face fines and other measures

The 2010 Livestock Identification and Registration Act and the regulations made the following year require that unidentified livestock will not be taken to livestock auctions or abattoirs.

Alternatively, if otherwise transported, the violators will be liable to 2m/- fine,"



he said, underlining that livestock identification, registration and subsequent follow up is essential for the sector's growth.

As it is a legal requirement, every livestock keeper is required to have his livestock identified and registered, as the target is to identify and register 45.9m livestock.

Up to October 15, 4.1m cattle had been registered, just 10 per cent of the target, close to a year since the registration drive was launched, he said.

He alluded to numerous challenges explaining the low turnout, including the failure of local government authorities in allocating adequate funds for the exercise.

Herders were complaining over the 1,750/- charge for cattle and donkey earrings and

TURN TO PAGE 2



**Swissport Tanzania executive director Mrisho Yasini (L) pictured in Dar es Salaam at the weekend presenting an ultrasound machine to CCBRT (Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania) Hospital CEO Brenda Msangi.** Photo: Correspondent Jumanne Juma

The Guardian Page no. 2.

# Livestock registration nears end, cattle keepers facing fines, losses

FROM PAGE 1

1,000/- charge for sheep and goats, he elaborated.

There was a poor understanding of the idea with herders on identification earrings, after the year-long drought since July 2021 which harmed livestock in various areas, he stated.

Mbeya Region is leading for livestock identified and registered, with upwards of one million animals, he said, appealing to local government authorities to take up their responsibilities to coordinate the exercise.

Livestock experts have to persist in education and mobilization of herders to have their livestock branded, he stated, pointing at sustainability benefits of the branding exercise.

Livestock identification, registration and follow up are essential for preventing infectious livestock diseases, he pointed out. It enhances the livestock market value, enabling access to insurance or loans for herders while locating stolen livestock if the need arises, he added.